Kitabu cha Ezra

MAZINGIRA YA EZRA NA NEHEMIA

Inaonekana kama wakati wa Agano la Kale vitabu vya Mambo ya Nyakati, Ezra na Nehemia viliunganishwa kuwa mfululizo wa habari. Kwa njia hiyo habari za Ezra zinaanza wakati ule ule ambapo habari za Mambo ya Nyakati zinamalizika.

Wakati huo ulikuwa mwaka wa 538 k.K. Waajemi walikuwa wameshinda Babeli muda mfupi uliopita, na mfalme wa Uajemi, Koreshi, alikuwa ametangaza amri iliyowapa Wayahudi uhuru wa warudi katika nchi yao (yaani mpaka wakati huo walikuwa wafungwa huko Babeli) (2 Nya 36:22-23; Ezra 1:1-4). Wakati uliofuata unajulikana kuwa wakati wa baada ya kifungo cha Babeli (post-exilic period). Vitabu sita vya Biblia, yaani vitatu vya historia na vitatu vya manabii, vinahusika na wakati huo. Muhtasari wa matukio unaotolewa hapa chini unataka kusaidia kuelewa vitabu hivyo zaidi.

Maelezo: Tangu wakati huo Waisraeli kwa kawaida walijulikana kuwa Wayahudi. Miaka kama 200 hivi ya awali watu wa ufalme wa kaskazini walipelekwa kifungoni katika mataifa mbalimbali, wengi wao wakapoteza ufahamu wa utaifa wao. Lakini watu wa ufalme wa kusini, yaani wa Yuda, walipopelekwa kifungoni Babeli baadaye, walihifadhi ufahamu wa utaifa wao. Watu hao wa Yuda waliitwa 'Wa Uyahudi', jina lililofupishwa kuwa *'Wayahudi',* Watu wengi zaidi waliorudi Palestina kutoka Babeli walikuwa wa ufalme wa kusini, kwa hiyo waliweza kuitwa Waisraeli au Wayahudi. Matengano ya Israeli hayakuendelea, kwa hiyo majina mawili, pamoja na jina la Waebrania, yaliweza kutumiwa kwa watu wale wale (Yer 34:9; Yn 1:19, 47; 2 Kor 11:22; Gal 2:14).

Kurudi kwa watu wa kwanza kutoka kifungoni

Kufuatana na amri ya Koreshi ya mwaka wa 538 k.K., Wayahudi walirudi Yerusalemu kwa maelfu na maelfu. Walikuwa na viongozi wao wa Kiyahudi, yaani Zerubabeli aliyekuwa kiongozi tangu wakati wa kifungoni na kuhani mkuu Yoshua (au Yeshua), lakini wote waliendelea kuwa katika ufalme mkuu wa Uajemi, na hivyo walikuwa chini ya utawala mkuu wa wafalme wake. Jiji la Yerusalemu lilikuwa katika mkoa uliojulikana kuwa *"Ng'ambo ya Mto"* (au *"Magharibi ya Frati"*), ulioanza katika Mto Frati na kuendelea mpaka Bahari ya Kati (Ezra 4:10, 16; 7:21, 25).

Muda mfupi baada ya kufika Yerusalemu, Wayahudi walianza kazi ya kujenga hekalu upya. Madhabahu iliwekwa mahali pake tena, na katika mwaka wa pili misingi ya hekalu ikawekwa (Ezra 3:1-3, 8-10). Lakini wakati huo maadui walianza kuwapinga wajenzi wakasababisha kazi yote ya ujenzi iahirishwe kwanza (Ezra 4:1-5, 24).

Manabii Hagai na Zekaria

Kwa muda wa miaka 16 hivi haikufanyika kazi yo yote katika ujenzi wa hekalu (Ezra 4:24). Kisha, mwaka wa 520 k.K., Mungu aliwaita watu wawili miongoni mwa Wayahudi walioishi Yerusalemu ili wawaamshe watu na kuwahamasisha waendelee na kazi yao ya hekalu, wala wasilegee tena mpaka wamalize kazi zote. Watu wale wawili walikuwa manabii Hagai na Zekaria (Ezra 5:1-2; Hag 1:1; Zek 1:1).

Mara watu walipoanza kazi ya ujenzi tena, upinzani mpya ulitokea (Ezra 5:3). Jambo hilo likawekwa mbele ya mfalme wa Uajemi aliyeitwa Dario (Koreshi alikuwa amekufa kabla ya miaka michache). Baada ya kuchunguza jambo hilo vizuri, Dario aligundua kwamba Koreshi alikuwa ametoa ruhusa ya kujenga hekalu. Kwa hiyo yeye Dario akaandika amri mpya iliyothibitisha ile ya kwanza ya Koreshi, ambayo iliruhusu kazi ya kujenga hekalu iendelee (Ezra 6:6-12).

Mahubiri ya Hagai ya kuamsha watu yalileta matokeo ya haraka, na baada ya muda mfupi Wayahudi walikuwa katika kazi yao tena ya kujenga hekalu. Nabii Zekaria akamwunga mkono Hagai, akitoa mafundisho marefu zaidi yaliyokusudiwa kuleta mabadiliko ya kiroho katika maisha na matumaini ya watu. Miaka minne baada ya kuanza kazi hiyo tena, hekalu lilimalizika (mwaka wa 516 k.K.; taz. Ezra 6:14-15; 4:24).

Kitabu cha Esta

Mfalme aliyetawala baada ya Dario alikuwa Ahasuero, ambaye pia alijulikana kuwa Xerxes I. Alitawala tangu 486 hadi 465 k.K. Yeye ndiye mfalme aliyehusika na habari za kitabu cha Esta.

Kurudi chini ya uongozi wa Ezra
Katika mwaka wa 465 k.K. Artashasta (au Artaxerxes) alikuwa mfalme wa Uajemi badala ya Ahasuero (au Xerxes I). Katika mwaka wa saba wa utawala wake (yaani 458 k.K.), aliandika amri iliyompa Ezra mamlaka na fedha kwa kurudi Yerusalemu na kutekeleza matengenezo ya huko (Ezra 7:1, 7, 13).

Kutokana na uchunguzi wa tarehe zinazohusika, inaonekana kwamba matukio yaliyoandikwa katika mafungu ya kwanza ya kitabu cha Ezra (k.mf. matukio yaliyohusika na Zerubabeli, Yoshua na kujengwa upya kwa hekalu), kwa kweli yalikuwa kabla ya kuzaliwa kwake Ezra. Bila shaka mwandishi wa kitabu cha Ezra alichunguza barua, hati na ripoti za historia nyingi ili kuandaa mambo mengi ya sehemu ya kwanza ya kitabu chake. Inatupasa kusoma zaidi ya nusu ya kitabu mpaka tunapopata habari za wakati wa Ezra mwenyewe. Kurudi kwa Ezra kulikuwa kama miaka 80 baada ya Zerubabeli. Watu wa Yerusalemu walikuwa kizazi kingine kuliko wale waliorudi pamoja na Zerubabeli.

Ezra alikuwa kuhani na mwandishi aliyejua sana sheria ya Mungu (Ezra 7:6, 12). Zamani za kale mwandishi alikuwa mtu aliyenakili sheria ya Mungu kwa watu waliotaka kuisoma, lakini baada ya kifungo cha Babeli alikuwa mtu wa maana au mtaalamu ambaye uamuzi wake katika mambo ya kidini uliheshimiwa sana. Katika miaka ya baadaye waandishi walizidi kupata nguvu na ushawishi katika Israeli, ambapo manabii walipungua kwa idadi na hata ushawishi wao.

Hata hivyo, Ezra alikuwa mtu aliyetumwa na Mungu. Yeye hakusoma sheria tu, bali pia alieleza maana yake, ili kitabu cha sheria kiwe cha mafundisho ya watu jinsi ya kufuata mambo ya maisha yao ya kila siku (Ezra 7:10; Neh 8:8). Hapa tunaweza kuona asili ya mipango ya dini ya Kiyahudi iliyoendelezwa na waandishi wa baadaye. Lakini mifano ya dini hiyo ya wakati wa Yesu inaonyesha kwamba ilitofautiana sana na aina ya maisha ya kidini iliyofundishwa na Ezra.

Kurudi chini ya uongozi wa Nehemia
Katika mwaka wa 20 wa utawala wake, Artashasta alitoa amri ya pili iliyowaruhusu Wayahudi wengine warudi Yerusalemu kwa msaada wa fedha nyingi za serikali, wakati huo wakiongozwa na Nehemia (445 k.K.). Hekalu la Yerusalemu lilikuwa limemalizika zaidi ya miaka 70 iliyopita, lakini jiji lenyewe bado ilikuwa na hali ya kusikitisha, wala ukuta uliozunguka jiji lote ulikuwa haujajengwa upya. Ilikuwa kwa kusudi la mradi huu wa ujenzi wa ukuta kwamba Nehemia alipata amri na msaada kutoka kwa Artashasta (Neh 2:1-8).

Ezra alikuwa amerudi Yerusalemu miaka 13 kabla ya Nehemia. Marekebisho yake yalikuwa na matokeo madogo tu, wala haikuwa mpaka baada ya kufika kwake Nehemia na kuwa Liwali mkuu wa Yerusalemu, marekebisho yale yalipoleta matunda kwa wenyeji kwa jumla. Watu wale wawili walifanya kazi pamoja, wakiwaongoza watu wamrudie Mungu (Neh 8:9). Nehemia aliishi Yerusalemu kwa muda wa miaka 12 kabla ya kurudi tena Uajemi (Neh 2:1; 13:6). Baada ya muda akarudi tena Yerusalemu (Neh 13:6-7). Kitabu cha Nehemia katika Biblia yetu kinaeleza matendo makuu ya Nehemia jijini Yerusalemu.

Nabii Malaki
Inafikiriwa sana kwamba ilikuwa wakati ule ule wa marekebisho ya Ezra na Nehemia baada ya kifungo cha Babeli ambapo nabii Malaki alitoa ujumbe wake. Tarehe au wakati wa unabii wake haviwezi kupangwa kwa uhakika, lakini dhambi alizozilaumu zilifanana na zile ambazo Ezra na Nehemia walipaswa kushughulika nazo. Watu walikuwa wametazamia kwamba, kwa sababu walirudi katika nchi yao na kujenga hekalu lao, wangefurahia baraka za Mungu zisizokuwa na mwisho. Mategemeo hayo hayakutimizwa na matokeo yake, watu walianza kutia shaka kama Mungu aliwaangalia kweli. Malaki alijibu kwamba sababu ya ukosefu wa baraka za Mungu ilikuwa upande wao wala si kwa Mungu. Kwa njia ya dhambi zao walikuwa wameweka vizuizi vilivyowazuia kufurahia upendo wa Mungu (Mal 1:2,6-7; 2:17; 3:7-8).

Kitabu cha Malaki kinafikisha huduma ya unabii wa Agano la Kale kwa Israeli katika mwisho wake. Miaka 400 ilipita mpaka sauti ya nabii iliposikika tena katika Maandiko, yaani sauti ya mtu aliaye nyikani, "Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake" (Mk 1:3).

MUHTASARI WA MATUKIO

k.K	**Wafalme wa Uajemi**	**Matukio**
539	Koreshi	Koreshi ashinda Babeli (Dan 5:30-31) Amri ya Koreshi: Kurudi kwa Serubabeli (Ezra 1:1; 2:2)
538		Kuanza ujenzi wa hekalu (Ezra 3:1-3, 8-10)
537		Kuahirisha ujenzi wa hekalu (Ezra 4:1-5:24)
530	Kambyses	Atawazwa
521	Dario I	Atawazwa
520		Unabii wa Hagai na Zekaria (Ezra 5:1-2; Hag 1:1; Zek 1:1) Amri ya Dario kujenga hekalu (Ezra 4:24; 6:6-12)
516		Kumalizika kwa hekalu (Ezra 6:14-15)
486	Xerxes I	Atawazwa (pia Ahasuero) (Esta 1:1)
465	Artashata	Atawazwa (pia Artaxerxes I)
458		Amri ya 1 ya Artashata: Ezra arudi (Ezra 7:1, 7, 13)
445		Amri ya 2 ya Artashasta: Nehemia arudi (Neh 2:1-8)
424		Mwisho wa utawala wa Artashasta

MUHTASARI WA KITABU CHA EZRA

1:1-2-70 Kurudi kwa Zerubabeli
3:1-6:22 Kujengwa upya kwa hekalu
7:1-8:36 Kurudi kwa Ezra
9:1-10:44 Matatizo ya ndoa za mchanganyiko